## Ikiwa una joto jingi ya 100.4ºF (Selsiasi 38º) au zaidi:



1. **Mpigie simu daktari wako wa saratani mara moja** - hata ikiwa ni wikendi, sikukuu au usiku wa manane.
   Usinywe dawa zinazopunguza joto mwilini kama vile: aspirini, acetaminophen (Tylenol), ibuprofen (Advil, Motrin), au naproxen (Aleve) bila idhini ya daktari wako.

2. Ikiwa hutapigiwa simu baada ya dakika 20, nenda kwa Idara ya Dharura iliyo karibu nawe (Emergency Department, ED). Piga simu kwa ofisi ya daktari wako tena na uwaambie ED unakoenda.

3. Ukienda kwa ED, mara tu unapofika mwambie mfanyakazi wa ED anayewasajili wagonjwa **na** muuguzi anayefanya tathmini ya kwanza:

   - kuwa unapokea matibabu ya saratani
   - jina la daktari wako wa saratani
   - kuwa una joto jingi na hali yako ni ya dharura

**Ikiwa una joto jingi, hakikisha kuwa unamwambia mfanyakazi wa ED anayewasajili wagonjwa na muuguzi anayefanya tathmini ya kwanza mara moja.** Joto jingi inamaanisha kuwa unaweza kuwa na maambukizi. Hili linaweza kuwa hali ya kutishia maisha na unapaswa kumwona daktari haraka.

Ikiwa daktari wako anadhani kuwa wewe ni mgonjwa sana, anaweza kukuambia uende ED kwa ambulensi. Ikiwa atapendekeza hivyo, ni kwa usalama wako.

Usisahau kumpa mfanyakazi wa ED nakala ya orodha ya dawa zako.

**Daktari wangu:** ______________________________________________

**Nambari ya simu ya daktari wangu:** ___________________________

**Piga 911 ukiwa na matatizo yoyote ambayo unahisi kuwa ni ya dharura.**

Ukipiga simu wakati ofisi ya daktari wako imefungwa, unapaswa kuunganishwa na huduma yetu ya kujibu simu. Ikiwa huwezi kufikia UH Seidman Cancer Center **baada ya saa za kazi, wikendi au sikukuu,** unaweza kupiga simu kwa huduma ya kujibu simu moja kwa moja kwa 1-877-669-2902.

# Piga simu kwa daktari wako mara moja ikiwa una:

### Dalili za maambukizi ambazo zinaweza kujumuisha:

- Joto jingi ya 100.4°F (38ºC) au zaidi
- Kutetemeka, kuhisi baridi au kutokwa na jasho ambayo inaanza au kuzidi kuwa mbaya
- Wekundu, uchungu, kutokwa na usaha, maumivu au uvimbe katika sehemu yoyote, ikiwa ni pamoja na vidonda, vifaa vya kuwekea dawa kwenye mishipa na sehemu za IV.
- Matatizo ya kupumua ambayo yanaanza au yanazidi kuwa mabaya
- Vipele au vidonda vinavyotokea kwenye ngozi yako
- Maumivu ya koo, vidonda vinavyotokea mdomoni au mabaka meupe mdomoni mwako
- Maumivu ya sinus, shinikizo au kufungana pua
- Kutapika
- Mkojo wenye damu au wenye rangi nyeupe
- Haja ya mara kwa mara ya kukojoa au hisia ya mchomo unapokojoa
- Kikohozi kinachoanza, mabadiliko ya kikohozi au kikohozi chenye kamasi kijani au njano (kohozi)
- Kutokwa na majimaji ukeni au kuwashwa ambayo si ya kawaida kwako
- Shingo ngumu
- Kwenda choo mara 3 au zaidi chenye majimaji ndani ya masaa 24 (kuhara)
- Maumivu mapya
- Kuchanganyikiwa au kuhisi usingizi sana au kutotulia bila sababu

### Sababu zingine za kumpigia daktari wako:

- Kushindwa kula au kunywa kwa masaa 12
- Kuanza kutokwa na damu mpya au michubuko
- Mabadiliko mapya ya ngozi, upele au malengelenge
- Maswali au wasiwasi
- Dalili au athari mpya au zinazozidi kuwa mbaya zaidi

**Piga 911 ukiwa na matatizo yoyote ambayo unahisi kuwa ni ya dharura.**